

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mkuuwa TAKUKURU (M)

KINONDONI,

S.L.P 90397,

KinondoniSimu : 222170852

Nukushi 2170963

TAARIFA KWA UMMA

TAKUKURU KINONDONI, 11/09/2019

KATIBU WA KAMATI YA URASIMISHAJI NYAKASANGWE
AFIKISHWA MAHAKAMANI

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (M) wa Kinondoni – Jijini Dar Es Salaam, leo tarehe 11/9/2019 inamfikisha mahakamani Bwana NERBERT MALEVU (33) mkazi wa NYAKASANGWE Kata ya WAZO Dar es Salaam na Katibu wa Kamati ya Upimaji wa viwanja katika Mtaa wa Nyakasangwe kwa kosa la kuomba rushwa ya shilingi milioni mbili na laki tano (Tsh.2,500,000/=) na kupokea rushwa ya shilingi laki tano (Tsh. 500,000/=) kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007.

Ilidaiwa kuwa mnamo tarehe 14/08/2019, Bwana Nerbert Malevu alimtaka mtoa taarifa (jina limehifadhiwa) ampatie shilingi milioni mbili na laki tano (Tsh. 2,500,000/=) ili aweze kumpatia sehemu ya kiwanja ambacho kilikuwa cha mtoa taarifa kabla ya upimaji na kwa madai kuwa sehemu ya kiwanja hicho kiligaiwa kwa mtu mwingine baada ya upimaji. Kitendo hiki ni kinyume na taratibu na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/ 2007.

Mlalamikaji alitoa taarifa TAKUKURU (M) Kinondoni tarehe 16/08/2019 ambapo uchunguzi ulifanyika na kubaini kuwa tuhuma hizo ni za kweli.

TAKUKURU (M) wa Kinondoni iliandaa mtego wa rushwa na kumkamata mtuhumiwa tarehe 20/08/2019 majira ya saa10 jioni eneo la Mwenge Lukani Pub baada ya kupokea shilingi laki tano (Tshs 500,000/=).

Aidha, katika tukio lingine; TAKUKURU (M) Kinondoni leo inawafikisha mahakamani watuhumiwa wengine wawili Bw. OMARY MOHAMED ABDALAH (40) aliyekuwa Hakimu Mahakama ya Mwanzo Magomeni na mkazi wa Kijitonyama kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya shilingi Laki saba na elfu tatu (Tshs. 703,000/=) na Bw. GEORGE JOSEPH BARONGO (37) Mfanyabiashara na mkazi wa Kibamba kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya shilingi Laki nne na elfu tisini na nane (Tshs. 498,000/=) kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007.

Ilidaiwa kuwa mnamo tarehe 12/02/2017 Bwana OMARY MOHAMED ABDALAH alimtaka mtoa taarifa (jina limehifadhiwa) ampatie shilingi milioni moja (Tsh. 1,000,000/=) ili aweze kumsaidia kwenye kesi ya Mirathi iliyokuwa mbele yake kinyume na utaratibu.

Mlalamikaji alitoa taarifa TAKUKURU (M) wa Kinondoni tarehe 01/03/2017, uchunguzi ulifanyika na kubaini kuwa tuhuma hizo ni za kweli.

Uchunguzi dhidi ya tuhuma zote mbili umekamilika na watuhumiwa wanafikishwa katika Mahakama ya (W) ya Kinondoni leo tarehe 11/09/2019 kujibu tuhuma zinazowakabili.

Mkuu wa TAKUKURU (M) Kinondoni Bi. THERESIA MNJAGIRA anatoa wito kwa watumishi wa Umma na Sekta Binafsi wanaodhani hawawezi kutoa huduma bila ya kuomba na kupokea rushwa, waache tabia hiyo kwani kuomba na kupokea rushwa ni makosa ya jinai na kwa wale watakao kaidi TAKUKURU itaendelea kuwachukulia hatua kali za kisheria bila huruma wala kumwonea haya mtu yeyote na anawasihi wananchi kuendelea kutoa taarifa pale wanapodaiwa rushwa kwa lengo la kupatiwa huduma kwani kupata huduma bila kutoa rushwa ni haki ya kila mwananchi.

Aidha, anawahimiza wananchi kuhudhuria kwa wingi kwenye vikao vya maandalizi ya urasimishaji wa viwanja ili kupata elimu juu ya taratibu za urasimishaji kwa lengo la kuondoa mwanya wa watendaji wachache wasio waadilifu kutumia udhaifu wa kutojua taratibu kuomba na kupokea rushwa

**IMETOLEWA NA:
MKUU WA TAKUKURU
MKOA WA KINONDONI
T.MNJAGIRA**